


Mchungaji Tony Alamo    Taifa la Kikristo la Alamo    Toleo 12700

# KUWA NA KRISTO NDANI YAKO



*Maelezo ya picha: Mchungaji Alamo angebatiza katika bahari ya Pasifiki kuanzia asubuhi na mapema hadi machweo ya jua hata usiku.* *Picha 1971*

**na Tony Alamo**

Jinsi tunavyozidi kumfahamu YESU zaidi, tunafahamu kwamba YEYE ni zaidi ya kila kitu. Kama tukimfuata KRISTO, tutaishi maisha tofauti na yale ulimwengu unaoyataka. Mateso tunayopata ni beji yetu ya heshima.

Kumwona YESU ni kumwona BABA.[1] "Filipo AKAMWAMBIA, BWANA, utuonyeshe BABA, yatutosha. YESU akamwambia, Mimi nimekuwepo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona MIMI amemwona BABA; unasemaje sasa, utuonyeshe BABA?" (Yohana 14:8-9).

Sisi wanadamu tunapaswa kuuliza kila jambo kwa kupitia NENO la MUNGU.[2] "Yeye anikataaye MIMI, na asiyeyakubali maneno YANGU, anaye amhukumuye; NENO hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho" (Yohana 12:48).

Daima mshukuru MUNGU kwa kila ulicho nacho.[3] Mwombe MUNGU akutie nuru kama alivyo YEYE. NENO LAKE hututia nuru kuhusu jinsi tunavyofaa kutembea katika NENO la MUNGU, ROHO MTAKATIFU, si tu siku ya Sabato pekee, lakini kila siku, kwa sababu kila siku ni Sabato.[4] Tunapumzika, Sabato, katika BWANA daima tukiacha njia zetu mbaya za kale (Waebrania 4:1-11).

Moyo wangu u katika Moto Mtakatifu kwa ajili ya ROHO MTAKATIFU. Uwe radhi kuwasaidia wengine kuubeba msalaba (Wagalatia 6:2). YESU alikuja kwa ajili ya wagonjwa na wala sio wenye afya! YESU alisema, "Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuwaita wenye haki, bali wenye dhambi" (Marko 2:17).

Wakatoliki wanaamini kuwa kuna hukumu mbili, ya kwanza ikiwa ni pagatori. Hii si kweli. Hakuna pagatori![5] NENO LA MUNGU linasema, "Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja na baada ya kufa hukumu [hukumu moja, hakuna kuzaliwa katika mwili mwingine]" (Waebrania 9:27). Maisha ya milele ni milele. Wakatoliki wanaamini mno katika umizimu na uzushi.

Ikiwa tumezaliwa upya, hatutendi dhambi, kwa sababu yeye atendaye dhambi ni wa Ibilisi.[6] "Atendaye dhambi, ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo" (1 Yohana 3:8). Sisi si watenda dhambi, bali wana wa MUNGU, uzao wa kifalme na kikuhani! "Kwa kuwa wote wanaoongozwa

*(Inaendelea ukurasa wa 2)*

**1** Yoh. 8:19, 10:30, 38, 14:7-11, 20, 23, 15:24, 17:21 **2** 1 Kor. 2:12-16, 6:1-4 **3** Zab. 100:4, Rum. 1:21, Efe. 5:2-5, 17-20, Kol. 1:10-13, 3:15-17, 1 Thes. 5:18, Ebr. 13:15 **4** Mat. 11:28-30, Rum. 8:1-6, Ebr. 4:9-10 **5** Mat. 25:31-46, Ebr. 9:27, 10:26-29, Ufu. 20:12-15 **6** Rum. 6:1-4, Gal. 2:16-20, 1 Yoh. 3:9

# KUWA NA KRISTO NDANI YAKO

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)*

na ROHO wa MUNGU, hao ndio wana wa MUNGU" (Warumi 8:14). "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya MUNGU, mpate kuzitangaza fadhili ZAKE yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru YAKE ya ajabu" (1 Petro 2:9).[7]

YESU anasema katika Mathayo 10:40, "Awapokeaye ninyi, anipokea MIMI; naye anipokeaye MIMI ampokea YEYE aliyenituma." YESU anasema, kama hunipokei mimi, Tony Alamo, ninayehubiri ukweli ambao NENO la MUNGU linasema, humkubali YESU, na humkubali BABA. Ukiangalia maneno anayosema YESU, wapo watu wengi wanaotupokea!

Watu hujidanganya kwa kusema kwamba MUNGU HAJIONDOI kamwe kutoka kwa watu ambao WAMEMFAHAMU;[8] lakini wapo wengi ambao wamemruhusu Shetani kuingia ndani yao na kuwatumia.[9] Uwepo wa MUNGU, ROHO WAKE, vimeondoka kwao bila ya wao kutambua![10]

Mema huwajia wenye subira. "Ninyi kwa subira yenu mtaziponya nafsi zenu" (Luka 21:19).

Kwa nini Wakatoliki wengi wanasema lugha ya Kilatini ni lugha takatifu wakati Biblia HAIKUANDIKWA na Warumi, ila wale waliokuwa Waebrania, waliozungumza Kiebrania, Kiaramu na Kiyunani cha Kiheleni, Kiyunani kilichokuwa kikizungumzwa na Wayahudi? Wayahudi ni watu ambao MUNGU aliwatumia kupokea ROHO ili kuandika Maandiko Matakatifu, SI Warumi hata kidogo! Petro hakuwahi kuwa Papa; alikuwa mmoja wa wanafunzi wa KRISTO, na pia mtume wa KRISTO.[11] YESU ametuonya kukaa mbali na manabii wa uongo na dini za uongo.[12] "Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wenye njaa kali" (Matayo 7:15).

MUNGU hakusema kamwe kwamba ndoa ni lazima iwe ya mke mmoja.[13] Watakatifu wengi walikuwa na mke zaidi

*(Inaendelea ukurasa wa 4)*

---

**7** Ufu. 1:6, 5:10 **8** Kumb. 31:16-18, Yos. 24:20, 1 Sam. 15:16-28, 1 Nya. 28:9, Eze. 33:12-13, Mat. 12:43-45, Lk. 9:62, Yoh. 15:6, Kol. 1:21-23, 2 Tim. 2:12, Ebr. 3:6-19, 4:1-11, 6:4-8, 10:25-31, 38-39, 2 Pet. 2:20-22, 2 Yoh. 9, Yud. 5-6, Ufu. 2:4-5, 3:2-3 **9** 1 Sam. 15:11, 16:14, 28:7-19, 31:1-6, 1 Fal. 3:3-14, 9:1-9, 11:1-34, Mat. 10:1-4, 26:14-16, Yoh. 13:1-2, 21-27, 18:1-5, 2 Pet. 2:18-22 **10** Amu. 16:20 **11** Mat. 10:2, Lk. 6:13-14, 1 Pet. 1:1, 2 Pet. 1:1 **12** Mat. 16:6-12, 24:11, 24, Mk. 8:15-21, 12:38-40, 13:21-23, Lk. 12:1-2, 20:46-47, 2 Pet. 2:1 **13** Kut. 21:10, Kumb. 21:15-17, 25:5-6, Amu. 8:30, 12:8-9, 13-14, 2 Sam. 3:2-5, 5:13-16, 12:7-8, Isa. 4:1, Mat. 5:17, 1 Tim. 4:1-3

# BARUA KWA MCHUNGAJI ALAMO

## Zambia

Mtumishi wa Mungu,

Naandika kumshukuru Mungu kwa kile anachokifanya katika maisha ya watu kwa njia ya maandiko yako; wengi wanaosoma maandiko haya, hutoa maisha yao kwa Bwana Yesu Kristo. Wengine bado wanaendelea na imani yao na wanazidi kumsifu Mungu kwa Baraka hizi. Bado ninao unyenyekevu na ukweli kwamba kwa njia ya maandiko yako nimekuwa mwinjilisti. Nawafikia watu wengi kwa neno hili la Mungu. Zaidi, nyumbani kwangu kumekuwa kituo ambamo watu wanaweza kujifunza neno la Mungu. Jambo hili linaninyenyekeza. Bwana huzidi kuwaleta watu kutoka kona mbalimbali mjini mwangu na maeneo mengine jirani kuja na kudai sehemu yao ya maandiko kwa ajili ya maombi na usambazaji. Nakuombea ili uweze kutuongeza vijuzuu vingi zaidi ili Mungu aweze kututumia kufikia maeneo mengi zaidi na zaidi. Kwa upendo tutumie maandiko zaidi ili tuweze kwenda sehemu nyingi zaidi kuifanya kazi hii tukufu ya kuwafikishia watu wengi zaidi injili, hasa kwa njia ya maandiko yako. Ni maombi yangu kwamba tuweze kufika kila kona ya nchi yetu, hata zile zilizosahaulika kuisambaza injili hii ulimwenguni humu. Kwa upendo tutumie nakala 3,000 za maandiko mema. Tutumie "Mifupa Mikavu," "Mlima mgumu," "Mjizatiti wenyewe," "Siri za Papa" kusoma na "Jihadharini na Baraka za Vatican" kwa wingi.

Tunaiombea huduma yako ili Bwana mwema azidi kukubariki jinsi unavyozidi kuufikishia ulimwengu wote habari njema. Binafsi nimeahidi kulitangaza neno hili ili niwe mmoja wa wanaohubiri Neno la Mungu.

Bwana mwema akubariki zaidi na zaidi na akutajirishe kwa uzima wa milele unapoendelea kutekeleza utume wake mkuu chini ya jua.

Mungu aibariki kazi ya mikono yako, huduma, na familia yako yote.

Wako katika Kristo,
Chileshe Amos Muselema
Mpulungu, Zambia, Africa

## Texas

Ndugu Mchungaji Tony Alamo,

Napenda muziki wa Kikristo wa injili. Ni wa kiroho sana. Natumaini utaucheza katika uamsho Bwana aliopanga. Inapendeza. Nakumbuka nilipokuwa nikikuangalia kwenye runinga nikiwa na umri wa miaka 12 au 15 hivi. Tukiwa ndugu sita tulitazama runinga moja. Nilikuona kwa dakika 3 tu na sikusahau hisia nilizokuwa nazo wakati nikitazama kipindi chako cha Kikristo.

Kwa upendo, Ysela El Paso, Texas

## Uganda

Moyo wangu uliinuliwa kutoka gizani nilipopata fursa ya kusoma jarida lako kutoka kwa rafiki yangu. Kwa hakika lilibadili maisha yangu. Naomba kupata majarida zaidi. Utakuwa ni mwanzo wa watu wa Uganda kuijua nguvu ya Mungu. Nimeokoka na ninampenda Mungu na ninataka kumtumikia maisha yangu yote. Mungu akubariki sana.

Ochean Headreen
Kampala, Uganda, Africa

## Ujerumani

Ndugu na Dada katika Kristo,

Napenda kuwasalimu katika jina lenye thamani la pekee la Bwana na Mwokozi wetu Yesu aliye Kristo. Vema, nimekuwa nikitembelea tovuti yako na ninaipenda sana. Nitafurahi sana kama itawezekana unitumie nyaraka nyingi za Kikristo (Jarida, Kitabu cha *Masihi,* Biblia) ili niweze kushiriki na wenzangu. Nimetembelea magerezani kuwaona wafungwa. Naamini watayapenda mafundisho haya. Nitafurahi sana kusikia kutoka kwako mara upatapo barua pepe hii.

Endelea kubarikiwa na Bwana.

Andre J. Schön — Sankt Augustin, Ujerumani

## Scotland

Kwa Huduma,

Unayo tovuti bora, tovuti halisi ya kiprotestanti. Tafadhali nitumie maandiko ya biblia.

Mungu awe nawe,

Mary — Glasgow, Scotland, UK

## India



*Mwinjilisti G. Prasanth Henry na mkutano wa washiriki, wasambazaji wa majarida ya Mchungaji Alamo katika Andhra Pradesh, India*

Ndugu mpendwa mtu wa Kristo,

Salamu nyingi kwako na kwa wapendwa wote wanaoshiriki katika huduma ya Kikristo ya Tony Alamo katika jina jema la pekee la Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo!

Natumaini umepokea picha za usambazaji wa maandiko; maandiko yako yananifaa sana katika maeneo yangu ya uinjilisti. Ni silaha yenye nguvu kumpatia Kristo roho nyingi. Hivyo nakuomba kwa upendo utume maandiko mara nyingi kwa ajili ya kuimarisha Ufalme wa Bwana katika nchi hii ya wasiomjua Mungu.

Tunakuombea, na watumishi wako wote, familia na kila ufanyalo kueneza ufalme wa Bwana katika dunia hii kupitia Huduma ya Kikristo ya Tony Alamo. Tunasubiri kusikia kutoka kwako mapema iwezekanavyo. Kujibu kwako kwa sala zitiazo nguvu kutatuimarisha kufanya kazi zaidi kwa utukufu wa Bwana.

Nashukuru nikitarajia mengi zaidi kutoka kwako.

Wako katika huduma

Mwinjilisti G. Prasanth Henry,

Harvest India Ministries

West Godavari District, Andhra Pradesh, India

## Pakistan

Ndugu Mchungaji Tony Alamo,

Mtukuze Mungu kwa kazi ya ajabu uliyokuwa ukiifanya. Nimepokea ujumbe wako kwa njia ya postmail. Ninafurahi kupokea ujumbe wako na ni wa kiroho, wenye hekima na umenikuza kiroho. Nimewagawia marafiki zangu kadhaa habari hizi, wamefurahi na wako tayari kusambaza Neno lililo hai la Mungu. Tafadhali endelea kunitumia kila mwezi na pia kitabu chako cha *Masihi*. Tafadhali uniombee mimi na marafiki zangu tunaposambaza habari hizi kwa roho zilizopotea. Mungu awabariki nyote. Kwa mara nyingine tena ahsante, Mchungaji Tony Alamo kwa kunitumia ujumbe wako.

M.M.

Karachi, Sindh, Pakistan




## Peru

*(Imetafsiriwa kutoka Kihispaniola)*

Ndugu,

Nimepokea ujumbe wako wa kaseti. Umekuwa Baraka kuu kwangu. Endelea kunitumia nyaraka za Biblia. Nahitaji Biblia zaidi na vitabu vya *Masihi,* majarida, na kila aina ya maandiko uliyo nayo, kwa sababu ni Baraka kuu kwetu. Mungu akubariki.

Ndugu, wanaendelea kutuma nyaraka zako. Usisahau kuhusu ombi langu binafsi la mafunzo yakinifu ya Biblia. Tunavuta roho nyingi kwa Kristo. Tunamwomba Mungu siku moja ututembelee hapa Peru. Mungu akubariki, ndugu.

Andres Chiroque Silva — Sullana, Peru

## KUWA NA KRISTO NDANI YAKO

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 2)*

ya mmoja.[14] Mwanamke anaweza kuwa na mume mmoja tu.[15] MUNGU, KRISTO, kamwe halaani hili, lakini analaani ushoga na ndoa za jinsia moja na kila aina ya ushoga![16]

YESU ni NENO la MUNGU (Yohana 1:1, 14). Kumjua YESU ni kulijua NENO la MUNGU. YESU, NENO, pia ni ROHO MTAKATIFU na Uzima wa Milele. Ili upate Uzima wa Milele, lazima KRISTO awe ndani yako kupitia ROHO MTAKATIFU. Ili hili litokee, Sali sala hii:

**BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mwenye dhambi[17] ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.[18] Ninaamini kwamba alikufa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.[19] Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kupitia nguvu za ROHO MTAKATIFU[20] na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikiliza maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.[21] Ninafungua mlango wa moyo wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.[22] Nioshe dhambi zangu kwa damu uliyoimwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,[23] hutanikataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia linasema hivyo.[24] NENO LAKO linasema hutamkataa yeyote na mimi nikiwemo.[25] Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.[26] Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonyesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kutotenda dhambi tena.[27]**

Baada ya kuokoka YESU alisema ni lazima kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa kwenye maji mengi kwa jina la BABA, MWANA na ROHO MTAKATIFU.[28] Kwa makini soma Biblia ya KJV, tafsiri ya Kiswahili ya The Bible League, Waenezaji wa Neno la Mungu tangu 1938 na ufanye inavyosema.[29]

BWANA anakutaka uwaambie wengine kuhusu wokovu wako. Unaweza kusambaza makala ya Injili ya mchungaji Tony Alamo. Tutakutumia makala hizi bila malipo. Tupigie simu ama ututumie barua pepe kwa habari zaidi. Mshirikishe na mtu mwingine ujumbe huu.

Iwapo unataka dunia yote iokolewe, kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, “Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghalani, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi” (Malaki 3:8-12).

---

**14** Mwa. 16:1-3, 25:6, 29:20-29, 30:4, 9-10, Kut. 2:21, Hes. 10:29, 12:1, Amu. 8:30-31, 1 Sam. 1:1-3, 25:39-44, 2 Sam. 3:2-5, 5:13, 15:16, 1 Nya. 1:32, 2:46-48, 14:3, 2 Nya. 13:21, 24:2-3, Hos. 1:2-3, 3:1-2 **15** Law. 20:10, Matt. 5:32, 19:3-9, Rum. 7:1-3, 1 Kor. 7:39 **16** Mwa. 19:1-13, 24-25, Law. 18:22, 20:13, Kumb. 23:17, Amu. 19:22-25, 1 Fal. 14:24, 15:11-12, Rum. 1:20-32, 1 Kor. 6:9-10, 1 Tim. 1:9-10, 2 Tim. 3:1-5, Yud. 7 **17** Zab. 51:5, Rum. 3:10-12, 23 **18** Mat. 26:63-64, 27:54, Lk. 1:30-33, Yoh. 9:35-37, Rum. 1:3-4 **19** Mdo. 4:12, 20:28, Rum. 3:25, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 5:9 **20** Zab. 16:9-10, Mat. 28:5-7, Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21, 10:17-18, 11:25, Mdo. 2:24, 3:15, Rum. 8:11, 1 Kor. 15:3-7 **21** Lk. 22:69, Mdo. 2:25-36, Ebr. 10:12-13 **22** 1 Kor. 3:16, Ufu. 3:20 **23** Efe. 2:13-22, Ebr. 9:22, 13:12, 20-21, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 1:5, 7:14 **24** Mat. 26:28, Mdo. 2:21, 4:12, Efe. 1:7, Kol. 1:14 **25** Mat. 21:22, Yoh. 6:35, 37-40, Rum. 10:13 **26** Ebr. 11:6 **27** Yoh. 5:14, 8:11, Rum. 6:4, 1 Kor. 15:10, Ufu. 7:14, 22:14 **28** Mat. 28:18-20, Yoh. 3:5, Mdo. 2:38, 19:3-5 **29** Kumb. 4:29, 13:4, 26:16, Yos. 1:8, 22:5, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Yak. 1:22-25, Ufu. 3:18

*Tafadhali wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambazo unaweza kuvutiwa nazo:*

**Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078**
**Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362**
**www.alamoministries.com • info@alamoministries.com**

*Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani ambao wanataka kumtumikia BWANA kwa mioyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.*

**Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.**
**Tafadhali wasiliana nasi kupitia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.**

**Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kiitwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.**

*Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo*
*Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kupitia meli.*
*Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhali tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.*

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)**
**USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

**Kwa wale ambao mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo mtachapisha tena, tafadhali jumuisha haki hii na usajili:**

© Hatimiliki Aprili 2011 Haki zote zimehifadhiwa World Pastor Tony Alamo ® Imesajiliwa Aprili 2011

SWAHILI—Vol. 12700—*To Have Christ in You*